

Wahyi (Tafsiri):

**MWONYAJI MMOJA ALIKUJA DUNIANI,
LAKINI DUNIA HAIKUMPOKEA.
BALI MUNGU ATAMPOKEA, NA
ATADHIHIRISHA UKWELI WAKE KWA
MASHAMBULIO MAKALI.**

WASIA

Mwandishi

**HADHRAT MIRZA GHULAM AHMAD
WA QADIAN
MASIHI ALIYEAHIDIWA NA IMAM MAHDI**

2007

ISLAM INTERNATIONAL PUBLICATIONS LIMITED

الوصية

Wasia

(Kiswahili rendering of 'Al-Wasiyyat' [Urdu])

Mwandishi: HADHRAT MIRZA GHULAM AHMAD WA QADIAN
MASIHI ALIYEAHIDIWA NA IMAM MAHDI

Kiswahili rendering of 'Al-Wasiyyat' [Urdu]

Mfasiri: Jamil R. Rafiq

© Islam International Publications Ltd

Urdu text first published in 1905

Many Urdu editions published since

Kiswahili translation published in Kenya in 2004

Reprinted in Tanzania in 2005

ISBN: 9987 – 8932 – 9 – 5

Present Kiswahili Edition (New translation) published
in 2007

Printed in Tanzania

Ahmadiyya Printing Press,

P. O. Box 376, Dar es Salaam, Tanzania

YALIYOMO

1	Kumhusu Mwandishi	i
2	Neno la Mbele	<u>iii</u>
3	Wasia	1
4	Nyongeza ya Wasia	31
5	Taarifa ya kikao cha kwanza cha Majlis Mu'tamadin Sadr Anjuman Ahmadiyya.	39

MAELEZO KUMHUSU MWANDISHI



Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad^{as} aliyezaliwa mwaka 1835 mjini Qadian (India) alijitolea kutaali Kurani Tukufu na kumwomba sana Mwenyezi Mungu na kushughulikia ibada yake. Alipoiona Islam ikishambuliwa vibaya sana kutoka kila upande na hali ya Waislamu kuwa ni duni mno na imani ikilegea na kuingiliwa na wasiwasi na dini ikififia kabisa, yeye akachukua jukumu la kuitetea Islam na kueleza kwa njia bora sana. Katika vitabu vyake vingi (Barahin-e-Ahmadiyya kikiwa kimojawapo kilicho mashuhuri sana), katika hotuba zake, maongezi na mijadala yake ya kidini na kadhalika alihakikisha kwamba Islam ndiyo imani hai na kwa kuifuata mtu anaweza kuungana na Mwumbaji wake na kupata

kuongea naye. Mafundisho yaliyomo katika Kurani Tukufu na sheria zilizoundwa na Islam zilikuwa na lengo la kumnyanyua mtu ili akamilike kikhulka, kiakili na kiroho. Alitangaza ya kuwa Mwenyezi Mungu Amenijalia kuwa Masihi na Mahdi kama ilivyotabiriwa ndani ya Biblia, Kurani Tukufu na Hadithi za Mtume^{sa} . Mnamo mwaka 1889 alianza kuchukua baiati za watu na kuwaingiza katika Jumuiya yake ambayo hivi sasa imekwisha imarika katika nchi 183 za dunia. Vitabu vyake 80 viliandikwa zaidi kwa Kiurdu, lakini baadhi yake vimo katika Kiarabu, na sehemu za baadhi ya vitabu ni kwa Kiajemi.

Baada ya Masihi Aliyehidiwa kufariki mnamo mwaka 1908, Hadhrat Maulawi Nuruddin^{ra} akawa Khalifa wake wa kwanza. Naye alipofariki katika mwaka 1914, Hadhrat Mirza Bashiruddin Mahmud Ahmad^{ra} aliyekuwa pia 'Mwana Aliyehidiwa' akawa Khalifa wake wa pili. Hadhrat Mirza Bashiruddin Mahmud Ahmad^{r.a} akaongoza Jumuiya akiwa Khalifa kwa muda wa miaka 52 hivi. Akafariki mnamo mwaka 1965, ndipo mwanaye mkubwa Hadhrat Mirza Nasir Ahmad^{r.a.} akachaguliwa kuwa Khalifa wa tatu. Huyu naye akafariki dunia katika 1982 baada ya kutoa huduma yake nzuri kwa miaka kumi na saba. Kisha nduguye mdogo Hadhrat Mirza Tahir Ahmadi^{r.h} akachaguliwa kuwa Khalifatul Masih IV. Yeye akaiongoza Jumuiya hadi ikaenea ilivyo na kuanza kujulikana kote duniani, na ndipo akafariki tarehe 19 Aprili 2003. Hadhrat Mirza Masroor Ahmad Khalifatul Masih V (a.t.b.a) ndiye Kiongozi wa sasa wa Jumuiya, naye ni kitukuu wa Mwanzilishi wa Jumuiya, Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad^{as}

NENO LA MBELE

Kijitabu ‘Al-Wasiyyat’ (Kiurdu) kilichoandikwa mnamo mwaka 1905 kinatoa habari njema ya Kudra ya Pili ya Mwenyezi Mungu kudhikirika kwa sura ya Ukhalifa, na kinaeleza kinaganaga utaratibu mkuu wa kufanya wasia kwa kuendeleza mbele miradi ya Islam na kuanzisha mava yaitwayo Bahishti Maqbarah.¹

Kijitabu hiki sasa kimefasiriwa kwa lugha ya Kiswahili na Jamil R. Rafiq, aliyekuwa Amir na Mbashiri Mkuu wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya nchini Tanzania na Kenya katika nyakati mbali mbali, kati ya mwaka 1968-1988, ambaye hivi sasa ni makamu wa Mwalimu Mkuu katika Jamia Ahmadiyya, Rabwah, Pakistan.

Zingatieni kwamba maneno katika mabano ya kawaida () na baina ya vistari kama hivi – ndiyo maneno ya Masihi Aliyehidiwa^{as}, lakini yaliyoandikwa katika mabano ya aina hii [] ndiyo maelezo ya mfasiri.

Mtakuta jina la Mtume Muhammad lafuatwa na^{sa}

¹ [Makaburi ya wale walio watu wa peponi machoni mwa Mwenyezi Mungu.]

ambayo ni kifupi cha Sallallahu alaihi wasallam, yaani Baraka na amani za Mungu ziwe kwake. Majina ya manabii na mitume wengine yafuatwa na^{as}. yaani alaihissalamu, amani iwe kwake.

Majina ya masahaba wa Mtume^{sa} na ya Masihi Aliyehidiwa yafuatwa na^{ra} yaani Radhiyallahu ‘anhu – Mungu Amwie radhi. Na alama ya rh. yamaanisha Rahmatullahi alaihi, rehema za Mungu ziwe kwake.

Waenezi

WASIA



Sifa zote njema ni za Mungu, Mola wa walimwengu. Na baraka na amani iwe juu ya Mtume Wake Muhammad na ahali zake na masahaba zake wote. Ama baadu, kwa kuwa Mwenyezi Mungu Amenipasha habari mfululizo kwa wahyi kwamba zama za kifo changu ni karibu – na kuhusu habari hiyo wahyi ulifululiza sana hata ukatetemesha msingi wa dhati yangu na kupoozesha maisha haya kwangu. Basi nikaonelea niwaandikie nasaha chache marafiki zangu na wale wote wapendao kufaidika na maneno yangu. Kwanza, basi, ningependa kuwaambia wahyi mtakatifu ambao ulinipasha habari ya kifo changu ukanihimiza kuandika wasia huu. Wahyi wenyewe ndio huu uliofunuliwa kwa Kiarabu, na baadaye wahyi wa Kiurdu nao utaandikwa:

قَرُبَ أَجَلُكَ الْمُقَدَّرُ. وَلَا نَبْقَى لَكَ مِنَ الْمُخْزِيَاتِ ذِكْرًا.
 قَلَّ مِيعَادُ رَبِّكَ. وَلَا نَبْقَى لَكَ مِنَ الْمُخْزِيَاتِ شَيْئًا. وَإِمَّا
 نُرِينَكَ بَعْضَ الدِّي نَعْدُهُمْ أَوْ نَتَوَفِّيَنَّكَ تَمُوتُ وَ أَنَا رَاضٍ
 مِنْكَ. جَاءَ وَقْتُكَ وَ نَبْقَى لَكَ الْآيَاتِ بَاهِرَاتٍ. جَاءَ

وَقُتِّكَ وَنُبْقِي لَكَ الْآيَاتِ بَيِّنَاتٍ. قَرُبَ مَا تُوعَدُونَ. وَ أَمَّا
 بِنِعْمَةِ رَبِّكَ فَحَدِّثْ. إِنَّهُ مَنْ يَتَّقِ اللَّهَ وَيَصْبِرْ فَإِنَّ اللَّهَ لَا يُضِيعُ
 أَجْرَ الْمُحْسِنِينَ.

Tafsiri: Kifo chako kimekaribia, nasi Hatutakuachia hata alama za yale yanayoweza kusababisha kukufedhehesha. Muda uliowekewa na Mungu umebaki kidogo, nasi Tutafutilia mbali upinzani wote wala Hatutabakiza chochote cha kukuletea fedheha. Na Tunaweza kukuonyesha kutimia kwa baadhi ya matabiri yetu kuwahusu wapinzani au kukufisha mapema. Utafariki ilhali Nitakuwa Nimekuridhia. Na Tutadumisha ishara zilizo wazi kuhakikisha ukweli wako. Iliyokuwa imeahidiwa ipo karibu. Waeleze watu neema ya Mola wako iliyo juu yako. Ashikaye ucha-Mungu na kusubiri, basi ajue kwamba Mungu Hatapoteza ujira wa watu wema.

Ikumbukwe hapa ya kwamba kauli hii ya Mwenyezi Mungu ya kuwa Hatutabakiza chochote cha kukuletea fedheha na kuvunja heshima ina maana mbili:

- (1) Ya kwanza ni kwamba upinzani wote unaoenezwa kwa nia ya kufedhehesha Tutaufutilia mbali hata kwamba alama zake pia hazitabaki.
- (2) Pili ni kwamba wale wanaopinga ambao hawaachi shari zao wala hawajizuii kunitaja vibaya Tutawaondoa duniani na kuwafutilia mbali, basi upinzani wao nao utafutika kwa sababu ya wao kuangamia.

Kisha baadaye Mwenyezi Mungu Akaniambia yafuatayo kuhusu kifo changu kwa lugha ya Kiurdu:

”بہت تھوڑے دن رہ گئے ہیں۔ اُس دن سب پر اُداسی چھا جائیگی۔ یہ ہوگا۔ یہ ہوگا۔ یہ ہوگا۔ یہ ہوگا۔ بعد اِس کے تمہارا واقعہ ہوگا۔ تمام حوادث اور عجائباتِ قدرت دکھلانے کے بعد تمہارا حادثہ آئے گا“

[Yaani: Siku chache sana zimebaki. Siku hiyo wote watajawa na huzuni. Hii itakuwa, hii itakuwa, hii itakuwa. Baadaye tukio kuhusu wewe litakulia. Baada ya kuonyesha mikasa yote na maajabu ya kudra, litafuata tukio kukhusu wewe].

Kuhusu mikasa hiyo elimu niliyojaliwa ni hii ya kwamba mauti yatatapakaa kila upande duniani. Na matetemeko yatatokea tena kwa nguvu sana nayo yatakuwa mfano wa Kiyama; yatafanya ardhi chini juu na maisha ya wengi yatakuwa machungu. Kisha watakaotubu na kuachana na dhambi, Mungu Atawahurumia. Kama alivyotabiri kila nabii, lazima yatendeke hayo yote. Lakini wale watakaojirekebisha nyoyo zao na kushika njia Anazopenda Mungu, hawatakuwa na hofu wala huzuni. Mungu Akiniambia Alisema:

”تو میری طرف سے نذیر ہے میں نے تجھے بھیجا تا مجرم نیکوکاروں سے الگ

کئے جائیں، اور فرمایا کہ ”دنیا میں ایک نذیر آیا پر دنیا نے اس کو قبول نہ کیا۔ لیکن

خدا اُسے قبول کرے گا اور بڑے زور آور حملوں سے اس کی سچائی ظاہر کر دیگا۔

میں تجھے استقدر برکت دوں گا کہ بادشاہ تیرے کپڑوں سے برکت ڈھونڈیں گے۔“

[U mwonyaji kutoka kwangu. Nimekutuma ili wenye dhambi watengwe mbali na watu wema.]

Na akasema:

[Mwonyaji mmoja alikuja duniani, lakini dunia haikumpokea. Bali Mungu Atampokea na kwa mashambulio makali Atadhihirisha ukweli wake.]²

Nitakubariki sana hata wafalme watatafuta baraka katika nguo zako.

Na kuhusu tetemeko lijalo litakalokuwa kali sana Amenispasha habari na kasema: “پھر بہا آئی خدا کی بات پھر پوری ہوئی”

[Msimu wa Rabiū – siku za kuchanua maua – ukaja tena na neno la Mungu likatimia mara nyingine.] Basi hakuna budi tetemeko moja kali kutokea. Lakini wakweli wamo katika amani kutokana na madhara yake. Hivyo kuweni wakweli; shikeni ucha- Mungu, ili mpate kusalimika. Mcheni Mungu leo ili muwe na amani katika hofu ya siku ile. Hakuna budi mbingu kuonyesha jambo na ardhi kudhihirisha kitu. Lakini wamchao Mungu wataokolewa.

Maneno ya Mungu yaniambia ya kuwa misiba mingi itadhihirika na maafa mengi yatashuka ardhini – mengine yatadhihiri katika uhai wangu na mengine baada yangu. Naye Ataipa Jumuiya hii maendeleo makamilifu – kadri fulani kwa mkono wangu na kadri fulani baada yangu.

² Kama dunia ingefumbua macho yake, ingeona ya kuwa nimedhihiri mwanzoni mwa karne. Na hadi sasa takriban robo ya karne ya kumi na nne imekwisha pita tayari. Na sawa na Hadithi za Mtume ^{s.a.w.} mwezi na jua vilipatwa katika Ramadhani wakati nilipokwisha dai [kuwa Mahdi], tauni pia iliambukiza nchini, na matetemeko pia yalikuja, na yatakuja zaidi. Lakini nasikitika waipendao dunia hawakunikubali.

Ni sunna ya Mwenyezi Mungu ambayo sunna hii tangu Alipomwamba binadamu katika ardhi Aliendelea kudhihirisha ya kwamba Yeye Huwasaidia manabii na mitume wake, na Huwapa ushindi kama Asemavyo ³ كَتَبَ اللَّهُ لَأَعْلَيْنَ أَنَا وَرُسُلِي Na ushindi muradi wake ni kwamba kama yanavyokuwa matakwa ya mitume na manabii ya kuwa hoja ya Mungu ikamilike ardhini na asiweze yeyote awaye kushindana naye, ndivyo Anavyodhihirisha Mwenyezi Mungu ukweli wao kwa ishara zenye nguvu, na kweli ile wanayotaka kuizagaza kote duniani Anapanda mbegu zake kwa mikono yao. Lakini Haitimizi kazi hii kikamilifu kwa mkono wao, bali kwa kuwafisha katika wakati ambao kidhahiri huwa na hofu ya ushinde, Huwapa wapinzani nafasi ya kucheka na kudhihaki na kufanya masihara na kuaibisha. Na pindi wanapokwisha kudhihaki, hapo Huonyesha mkono wa pili wa kudra yake na Huleta sababu ambazo kwa njia hizo hutimia miradi iliyobakia kadri fulani kutimia. Ndiyo kusema kwamba Hudhihirisha kudra ya namna mbili: (1) Kwanza, kwa mkono wa manabii wenyewe huonyesha mkono wa kudra yake. (2) Pili, katika wakati ambapo matatizo yanazuka baada ya kifo cha manabii na maadui hupata nguvu na hudhani mambo yameharibika na huwa na yakini kwamba sasa Jumuiya hii itafutika, bali na wanajumuiya nao huhangaika na kuvunjika moyo, na baadhi yao wenye bahati mbaya wanashika njia ya kuritadi, hapo Mwenyezi Mungu Hudhihirisha mara ya pili kudra yake yenye nguvu na kuimarisha Jumuiya iliyokuwa inaanguka.

³ (Tafsiri) Mungu Amekwisha andika ya kwamba Yeye na mitume wake watashinda [Mujadalah: 22]

Basi yule anayesubiri mpaka mwisho, huona mwujiza wa Mwenyezi Mungu, kama ilivyotendeka katika enzi ya Hadhrat Abu Bakr^{ra} Wakati huo kifo cha Mtume^{sa} kilipofikiriwa kutokea wakati usiofaa na mabedui wengi wakaritadi na masahaba kwa sababu ya huzuni kubwa wakawa kama kwamba wameshikwa na wazimu, hapo Mwenyezi Mungu kwa kumsimamisha imara Hudhrat Abu Bakr Siddiq^{ra} Akaonyesha mara ya pili onyesho la kudra yake na Akanusuru Islam iliyokurubia kufutika, na Akatimiza Aliyoahidi ya kwamba

4. **وَلْيَمَكِّنَنَّ لَهُمْ دِينَهُمُ الَّذِي ارْتَضَى لَهُمْ وَلِيُبَدِّلَنَّهُم مِّنْ بَعْدِ خَوْفِهِمْ أَمْنًا.**

Yaani, baada ya hofu Tutawaimarisha. Ndivyo ilivyofanyika katika zama za Hadhrat Musa^{as}, ambapo yeye Hadhrat Musa^{as} kabla ya kuwafikisha wana wa Israeli huko Misri na Kanani sawa na ahadi yake akafariki njiani. Kifo chake kilizusha maombolezo makubwa ilivyoenezwa katika Torati. Wana wa Israeli waliendelea kuomboleza siku arobaini kwa huzuni ya kifo hiki kilichotokea wakati usiofaa na kuaga kwa Hadhrat Musa^{as} ghafla. Kadhalika ikatokea kwa Hadhrat Isa^{as}. Wakati wa tukio la msalaba, wanafunzi wote wakatawanyika na mmoja miongoni mwao akaritadi pia.

Basi, enyi wapenzi, kwa kuwa hii ndiyo sunna ya Allah tangu kale ya kwamba Mwenyezi Mungu Huonyesha kudra mbili ili kuzikanyagilia mbali furaha

⁴ [An-Nur: 56]

mbili za bandia za wapinzani, hivyo haiwezekani sasa ya kuwa Mwenyezi Mungu Aziache sunna yake ya zamani. Kwa hiyo msihuzunike kwa habari niliyowaambieni wala nyoyo zenu zisifazaike, kwani hamna budi kuiona kudra ya pili vilevile. Na kuja kwake ni bora kwenu kwa sababu hiyo itadumu, nayo itaendelea bila kukoma mpaka Kiyama. Na hiyo kudra ya pili haiwezi kuja mpaka niondoke. Lakini niondokapo, hapo Mungu Atakutumieni hiyo kudra ya pili itakayodumu nanyi milele kama Mungu Alivyoahidi katika Barahini Ahmadiyya. Ahadi hiyo hainihusu mimi bali yawahusuni ninyi, kama Alivyosema kwamba Nitashindisha Jumuiya hii inayokufuata juu ya wengine hadi Kiyama. Basi hakuna budi mfikiwe na siku ya mimi kuagana nanyi ili baadaye iwadie ile siku iliyo siku ya ahadi ya kudumu. Mungu wetu huyu ndiye Mungu Atimizaye ahadi, Mwaminifu na Mkweli. Atawaonyesheni yote Aliyoahidi. Ijapokuwa hizi ni siku za mwisho za dunia na ndiyo zama za balaa nyingi kushuka, lakini hakuna budi dunia hii ibaki mpaka yote hayo yatimie Aliyoniambia Mungu. Mimi nimedhihirika nikiwa kudra moja kutoka kwa Mungu, nami ndimi kudra hasa ya Mungu na baada yangu watakuwapo wengine watakaokuwa onyesho la kudra ya pili. Hivyo basi, endeleeni kuomba mkiwa pamoja ili kuingoja kudra ya pili ya Mungu. Na yawapasa wanajumuiya wema wa kila nchi wakiwa pamoja kwamba wadumu kuomba ili kudra ya pili ishuke kutoka mbinguni na iwahakikishieni kwamba Mungu wenu ndiye Mungu Mweza hivyo. Fikirini mauti yenu kuwa karibu. Hamjui saa hiyo itawadia lini.

Na yawapasa watu wema waliotakasika wachukue baiati kwa jina langu baada yangu.⁵

Mwenyezi Mungu Anataka kwamba wote waishio katika makazi tofauti ya ardhi wakiwa katika Yoropa na Asia, wote walio na tabia njema Awavutie kwenye Umoja wa Mungu na kuwakusanya katika dini moja. Hiyo ndiyo shabaha ya Mwenyezi Mungu niliyotumwa kwayo. Basi ifuateni shabaha hii, lakini kwa upole, khulka njema na kukazania maombi. Na mpaka asimame yeyote akipata Roho Takatifu kutoka kwa Mwenyezi Mungu nyote mfanye kazi kwa pamoja.

Na yawapasa ninyi nanyi mpate sehemu katika Roho Takatifu kwa kujitakasa nafsi zenu, kwani ucha-Mungu wa kweli hauwezi kupatikana pasipo Roho Takatifu. Na kwa kutengana kabisa na tamaa za nafsi shikeni ile njia ya kupata radhi ya Mungu ambayo hakuna njia nyembamba zaidi kuliko hiyo. Msiangukie ladha za dunia, kwani hizo zatenganisha na Mungu; jichagulieni maisha ya uchungu kwa ajili ya Mungu. Uchungu ambao Anaoridhia Mungu ni afadhali kuliko ladha Anayokasirikia Mungu. Ushinde ule Anaoridhia Mungu

⁵ (Uchaguzi wa watu hao utategemea rai ya waaminio kwa pamoja. Basi yule ambaye juu yake waaminio arobaini watapatana, huyo atapaswa kuchukua baiati ya watu kwa jina langu. Yampasa huyo ajifanye mfano kwa wengine. Mungu Amenipasha habari ya kwamba Mimi Nitainua mtu mmoja kutoka katika dhuria yako kwa ajili ya Jumuiya yako. Nami Nitamchagua kwa ukaribu wangu na wahyi wangu. Na haki itazagaa kwa mkono wake, na watu wengi sana watapokea ukweli. Basi zisubirini zile siku. Na kumbukeni, kila mmoja anatambulikana katika wakati wake. Yawezekana yeye aonekane kuwa mtu wa kawaida kabla ya wakati wake ama apingwe kwa sababu ya mawazo yadanganyayo, kama mtu mkamilifu pia huwa tone tu la manii au pande la damu tumboni).

ni bora kuliko ule ushindi unaosababisha ghadhabu ya Mungu. Acheni mapenzi yale yanayosogeza karibu na hasira ya Mungu. Mkienda upande wake kwa usafi wa moyo, Yeye Atawasaidieni kwa kila njia, wala adui yeyote hataweza kuwadhuruni. Hamwezi kupata radhi ya Mungu kwa vyovyote mpaka mkiachana na ladha zenu na heshima zenu na mali zenu na kutokujali uhai wenu, mvumilie katika njia yake uchungu ulio mfano wa mauti. Lakini mkivumilia uchungu huo, mtakaa mapajani mwa Mungu kama mtoto mpenzi, na mtafanywa warithi wa wakweli waliopita kabla yenu, na mtafunguliwa milango ya kila neema. Lakini ni wachache walio wa aina hii. Mungu Alisema Akiniambia mimi: Taqwa (ucha-Mungu) ni mti unaopaswa kupandwa moyoni. Maji yale yakuzayo ucha-Mangu ndiyo yanayonyesheleza bustani nzima. Ucha-Mungu ni mzizi ambao kama haupo, basi hamna chochote wala lolote, lakini kama huo umebaki, basi kila kitu kipo salama. Mwanadamu afaidikaje na upuuzi wa kudai kwamba anamtafuṭa Mungu lakini hakanyagi hatua ya kweli. Angalieni, nawaambieni kweli kweli ya kwamba ameangamia yule mtu anayeichanganya dini na dunia hata kidogo. Na Jahanamu ipo karibu sana na yule ambaye matakwa yake yote siyo kwa ajili ya Mungu; bali mengine ni kwa Mungu na mengine kwa dunia. Hivyo, kama mnaichanganya dunia hata sawa na chembe katika shabaha zenu, ibada zenu zote ni bure kabisa. Maana hamfuati Mungu hapo, bali mwamfuata shetani. Msitazamie kwamba katika hali hii Mungu Atawasaidia. Bali m-wadudu wa dunia katika hali hii, na mtaangamia katika siku chache kama waangamiavyo wadudu. Na Mungu Hatakuwa ndani yenu, bali kwa kuwaangamizeni

Mungu Atafurahi. Lakini kama mtaziua tamaa za nafsi, hapo mtadhihiri ndani ya Mungu, na Mungu Atakuwa pamoja nanyi. Itabarikiwa ile nyumba mtakamoishi, na kuta zile zilizo za nyumba yenu zitashukiwa rehema ya Mungu. Na utabarikiwa mji anamoishi mtu wa aina hii. Kama uhai wenu na kifo chenu na kila mwendo wenu na upole wenu na hararra yenu itakuwa kwa ajili ya Mungu, na wakati wa kila uchungu na msiba hamtamjaribu Mungu wala hamtavunja uhusiano wenu naye, bali mtakanyaga mbele hatua, hapo nawaambieni kweli kweli ya kwamba mtakuwa kaumu maalumu ya Mungu. M wanadamu nilivyo mwanadamua mimi; na Mungu wangu ndiye Mungu wenu. Basi msipoteze bure vipawa vyenu vitukufu. Kama mkielekea kwa Mungu kikamilifu, sikilizeni, nawaambia sawa na matakwa ya Mungu kwamba mtakuwa kaumu teule ya Mungu. Tieni nyoyoni mwenu adhama ya Mungu. Na kirini Umoja wa Mungu – si kwa ulimi pekee, bali kwa kitendo ili Mungu Awadhihirishieni kwa kitendo upole wake na hisani yake. Epukaneni na inadi, na watendeeni wanadamu kwa huruma ya kweli. Shikeni kila njia ya wema, hamjui mtakubaliwa kutoka katika njia gani.

Mpate habari njema ya kwamba uwanja wa kumkurubia Mungu uko wazi. Kila kaumu inashughulikia kuipenda dunia, isilizingatie Analoliridhia Mungu. Wale wapendao kuingilia mlango huu kwa nguvu zao zote wanayo fursa ya kuonyesha vipawa vyao na kupata zawadi maalumu kutoka kwa Mungu. Msidhani kwamba Mungu Atawapotezeni bure. M-mbegu iliyopandwa ardhini kwa mkono wa Mungu. Mbegu hii itaota na kukua, yatatoka matawi yake kutoka kila upande na hatimaye itakuwa mti mkubwa. Basi amebarikiwa yule aiadiniye

habari hii wala asitishike na majaribio yajayo kati, kwani majaribio hayana budi kuja ili Mungu Awajaribu kwamba nani ndiye mkweli katika madai yake ya baiati na nani mwongo! Yule atelezaye kwa jaribio hatampa Mungu hasara yoyote, bali bahati yake mbaya itamfikisha Motoni. Kama asingezaliwa ingekuwa bora kwake. Lakini wale wote watakaosubiri ambao watatetemeshwa na misiba na kupigwa na dhoruba za misukosuko, na kaumu zitawacheka na kuwadhihaki na dunia itawatenda kwa karaha sana, hao mwishowe watapata ushindi, na watafunguliwa milango ya baraka. Mungu kasema Akiniambia ya kwamba niipashe habari Jumuiya yangu ya kuwa wale walioamini na imani yao haikuchanganyikana na tamaa za kidunia wala imani yao haikuchafuliwa na unafiki wala woga, na imani hiyo haikukosa daraja lo lote la utii, hao ndio watu Anaowaridhia Mungu, na Mungu Anasema ndio hao ambao hatua yao ndiyo hatua ya kweli.

Sikilizeni, enyi wasikiao, kwamba Mungu Anataka nini kutoka kwenu! Hii tu kwamba muwe wake pekee. Msimshirikishe naye yeyote, si huko mbinguni wala si hapa ardhini. Mungu wetu ndiye Mungu Aliye hai hata sasa jinsi Alivyokuwa hai hapo kabla, na Husema hata sasa Alivyokuwa Akisema zamani, na Husikia Alivyosikia katika zama zilizopita. Ni wazo potevu kwamba Yeye Anasikia siku hizi lakini Hasemi, bali Husikia na Husema pia. Sifa zake zote ni za tangu azali na zitadumu milele. Sifa yeyote haihiri wala haitaahiri abadani. Yeye ndiye Mmoja wa pekee Asiye na mshirika Ambaye hana mwana yeyote awaye wala mke. Ndiye asiye kifani ambaye hana anayefanana naye, wala hamna mtu yeyote anayehusika na sifa

yoyote iwayo kama Yeye. Na Ndiye ambaye hakuna Aliye sawa naye, ambaye hakuna anayeshirikiana naye katika sifa, ambaye hakupungukiwa nguvu yoyote. Yu karibu juu ya kuwa mbali; na Yu mbali japo Yu karibu. Huweza kujidhihirisha kimfano kwa waonao kashfi, lakini hana mwili wowote wala sura maalumu yoyote. Yu juu ya vyote, lakini hatuwezi kusema chini yake kuna chochote. Naye Yu juu ya Arshi (kiti cha enzi), lakini hatuwezi kusema kwamba Hayupo ardhini. Sifa zote kamilifu zimo ndani mwake, sifa zote njema hudhihirika kutoka kwake, na ndiye chemchem ya sifa zote. Amejikusanyia nguvu zote, na Yu chanzo cha neema zote, vyote hurejea kwake. Yu Mmiliki wa kila dola. Anao kila ukamilifu na ameepukana na kila aibu na udhaifu. Yeye pekee anapaswa kwamba waishio ardhini na mbinguni wafanye ibada yake. Hakuna kisichowezezana kwake. Roho zote na nguvu zao na chembe zote pamwe na nguvu zake vimeumbwa naye. Minghairi yake chochote hakidhihiriki. Hujidhihirisha kwa njia ya nguvu zake na kudra zake na ishara zake. Twaweza kumpata kwa njia yake Yeye Mwenyewe. Hujidhihirisha siku zote kwa wakweli na kuwaonyesha kudra zake. Hutambuliwa kwa njia hiyo, na kwa njia yake Yeye, njia Aipendayo Hujulikana. Huona bila macho ya kimwili, na Husikia pasipo masikio ya kimwili, na Husema pasipo ulimi wa kimwili. Kitu kisichokuwapo Hukiumba jinsi mnavyoona katika njozi kwamba Anaumba ulimwengu mzima pasipokuwa na msaada na kuwaonyesha kila mfile na kisichokuwepo kwamba chawepo. Ndivyo hivyo zilivyo kudra zake zote. Ni jahili tu anayezikana kudra zake. Ni kipofu tu yule asiye na habari ya nguvu zake zenye kina. Hufanya yote, na

Huweza kufanya yote isipokuwa mambo yale yaliyo kinyume cha shani yake au yaliyo dhidi ya ahadi zake. Yu wa pekee katika dhati yake na sifa zake na vitendo vyake na kudra zake. Kwa kumfikia milango yote imefungwa isipokuwa mlango mmoja uliofunguliwa na Furqan Majid (Kurani Tukufu). Hamna haja tena kufuata unabii wote na vitabu vyote mbalimbali vilivyokwisha pita, kwani Unabii wa Muhammad^{s.a.} umejikusanyia hivyo vyote. Pasipo njia hii, njia zote nyingine zimefungwa. Kweli zote zifikishazo kwa Mungu zimo ndani yake. Hakuna ukweli wowote mpya utakaokuja baada yake, wala hamna ukweli wowote wa zamani usiokuwamo ndani mwake. Hivyo unabii wote umeishia ndani ya unabii huu, na ndivyo ilivyopaswa, kwani kilicho na mwanzo, kina mwisho wake pia. Lakini Unabii huu wa Muhammad^{s.a.} haushindwi kutoa baraka zake zilivyo, bali unaupita unabii wowote mwingine katika baraka zake. Ufuasi wa unabii huu hufikisha mpaka kwa Mungu kwa njia sahihi kabisa. Na kwa kuufuata, Upendo wa Mungu na neema ya kuongea naye hupatikana zaidi sana kuliko ilivyopatikana hapo kabla. Lakini mfuasi wake mkamilifu hawezi kuitwa ‘nabii’ pekee, kwani ni kinyume cha heshima ya unabii mkamilifu mtimilifu wa Muhammad^{sa}. Naam, maneno ‘Ummati’ na ‘Nabii’, yote mawili pamoja, yaweza kuwa sawa kwake, kwani huku hakuna kuivunja heshima ya Unabii mtimilifu mkamilifu wa Ki-Muhammadi, bali mng’ao wa Unabii wake hudhihirika zaidi mno kwa baraka hiyo.*

* Hata hivyo, kumbukeni sana ya kwamba mlango wa unabii wenye sheria mpya umefungwa kabisa, wala hakuna baada ya Kurani Tukufu Kitabu chochote kifundishacho maamrishi mapya au kitanguacho amri ya Kurani Tukufu au kifutacho ufuasi wake; bali hiyo itafuatwa mpaka kiyama.

Na maongezi hayo (na Mungu) yakifikia upeo wake kwa hali na wingi wake hata kwamba hamna mle ndani yake uchafu wala kasoro, nayo yanaeleza bayana habari za ghaibu, hapo maongezi hayo huitwa kwa maneno mengine ‘Unabii’, na manabii wote wameafikiana juu yake. Basi isingewezekana kwa walioambiwa

كُنْتُمْ خَيْرَ أُمَّةٍ أُخْرِجَتْ لِلنَّاسِ [M umati bora uliotolewa kwa watu] na waliofundishwa dua اِهْدِنَا الصِّرَاطَ الْمُسْتَقِيمَ صِرَاطَ

الَّذِينَ أَنْعَمْتَ عَلَيْهِمْ [Tuongoze njia iliyonyoka, njia ya wale Uliowaneemesha] kunyimwa daraja hili la juu kiasi hiki kwamba hata mtu mmoja kati yao asingepata daraja hili. Katika hali hiyo usingetokea ubaya huu pekee ya kwamba Umati wa Muhammad^{sa} ungekuwa na kasoro na upungufu, na wote wangebaki kama vipofu, bali kasoro hii pia ingekuwapo ya kwamba nguvu ya Mtume^{sa} ya kutoa baraka ingepata ila, na nguvu yake takatifu ingeonekana kuwa pungufu. Isitoshe, na dua iliyofundishwa iombwe katika sala tano ingekuwa bure kufundishwa. Lakini upande mwingine kulikuwa na ubaya huu ya kwamba kama mtu yeyote wa umati huu angeweza kupata ukamilifu huu moja kwa moja pasipo kufuata nuru ya unabii wa Ki-Muhammad, hapo maana ya Khatmi Nubuwwat ingebatilika. Kwa hiyo, ili kukinga na ubaya wa namna hizo mbili, Mwenyezi Mungu Akawapa heshima ya maongezi yake makamilifu matimilifu matakatifu baadhi ya watu waliofikia daraja timilifu la kujipoteza katika dhati ya Mtume^{s.a.} pasipokuwa na pazia lo lote katikati, na muradi wa kuwa katika umati wake na maana ya ufuasi wake ilipatikana kitimilifu na kikamilifu ndani yao hata kwamba dhati yao

haikubaki kuwa dhati yao, bali ndani ya kioo cha hali yao ya kujifutilia mbali, dhati ya Mtume^{sa} ikadhihirika kama kivuli. Na upande mwingine wakajaliwa kuongea na Mungu kitimilifu na kikamilifu kama manabii wengine.

Basi, kwa njia hii baadhi ya watu juu ya kuwa katika umati wa Mtume^{sa} wakapata lakabu ya kuwa Nabii, kwani unabii wa aina hii hauko mbali na unabii wa Ki-Muhammad. Bali mkitafakari mtaona kuwa huo ndio unabii wa Ki-Muhammad tu uliodhihirika kwa njia mpya. Huo ndio muradi wa maneno Nabiyullah na Imamukum minkum aliyosema Mtume^{sa} kumhusu Masihi Mau'udi. Yaani yeye atakuwa nabii na pia atakuwa katika umati wangu. La sivyo, mwingine yeyote asiyetokana naye hawezi kukanyaga hapo. Amebarikiwa yule ayatambuaye maarifa haya ili asipate kuangamia. Mungu Alimfisha Isa^{as} kama aya safi iliyo wazi ya Mwenyezi Mungu

فَلَمَّا تَوَفَّيْتَنِي كُنْتَ أَنْتَ الرَّقِيبَ عَلَيْهِمْ

[Uliponifisha Ukawa Mchungaji juu yao. 5:118] inavyoshuhudia, ambayo muradi wake pamoja na aya zinazohusiana na aya hiyo ni kwamba Mungu Atamwuliza Nabii Isa siku ya Kiyama, 'Je wewe uliwafundisha wafuasi wako wakuamini wewe na mama yako kuwa miungu? Hapo yeye atajibu kwamba nilipokuwa kati yao nilikuwa shahidi juu yao na mchungaji wao, lakini Uliponifisha hapo sina habari kwamba wakaangukia upotevu gani. Sasa ni juu ya mtu kuifasiri aya

فَلَمَّا تَوَفَّيْتَنِي كُنْتَ أَنْتَ الرَّقِيبَ عَلَيْهِمْ kuwa 'Uliponifisha' au aking'ang'ania pasipo haki aifasiri 'Uliponinyanyua na kiwiliwili changu hadi mbinguni.'

Kwa vyovyote aya hii yahakikisha kwamba Nabii Isa^{as}. hatakuja mara ya pili duniani. Kwani kama angalikuwa amefika duniani mara ya pili kabla ya Kiyama na kuvunja msalaba, hapo isingaliwezekana kwa Isa aliyekuwa Nabii kuongopa waziwazi mbele ya Mwenyezi Mungu kwamba sina habari ya kuwa wafuasi wangu walishika itikadi potovu ya kunifanya mimi na mama yangu kuwa miungu. Je yule mtu ajaye duniani mara nyingine na kukaa hapa miaka arobaini akapigana na Wakristo aweza kusema uwongo mchafu mno kwamba mimi sina habari, ilhali anajiita Nabii? Basi ikiwa aya hiyo yamzuia Nabii Isa^{as}. asirudi mara ya pili – la sivyo ataonekana yu mwongo – na kama yeye yupo mbinguni na kiwiliwili chake na sawa na muradi wa aya hiyo hatashuka ardhini hadi siku ya Kiyama, je, basi, atafia huko huko mbinguni? Na kaburi lake litakuwa huko mbinguni?

Lakini kufia mbinguni ni kinyume cha aya **فِيهَا تَمُوتُونَ**

[Mtafia humu 7:26] Hivyo, ikathibitika kwamba yeye hakwenda mbinguni na mwili wake. Na kama Kitabu cha Mungu kimekwisha amua bayana, hapo kukipinga kitabu cha Mungu kama si uasi, ni nini tena?

Kama nisingalifika, kosa hili la ki-ijitihadi lingefaa kusamehewa, lakini baada ya mimi kufika kutoka kwa Mungu, na maana sahihi na ya kweli kujulikana tayari, kutokuachana na kosa hilo si njia ya waaminifu. Ishara za Mungu zikadhihiri kwa ajili yangu huko mbinguni na ardhini, na karibu robo ya karne pia imekwisha pita, na maelfu ya ishara zikadhihirika, na katika umri wa dunia elfu ya saba imekwisha anza, basi hata sasa kukataa kupokea haki ni ugumu gani huu wa moyo! Angalieni,

nasema kwa kupaza sauti ya kwamba ishara za Mungu bado hazijamalizika. Baada ya ishara ya tetemeko lile la kwanza lililotokea tarehe 4 Aprili 1905 ambalo lilitabiriwa mapema sana, Mungu Ameniambia tena kwamba katika siku za rabiū (siku za kuchanua maua) tetemeko jingine kali sana litatokea. Zitakuwa siku za rabiū. Haijulikani ni mwanzo wa rabiū miti inapochipua, au katikati yake au sehemu yake ya mwisho. Iliyoyofunuliwa na Mungu ni:

“پھر بہار آئی خدا کی بات پھر پوری ہوئی”⁶. Kwa kuwa tetemeko la kwanza lililotokea katika siku za rabiū, hivyo Mungu Akatoa habari ya kuwa tetemeko la pili nalo litatokea katika rabiū. Na kwa kuwa miti yaanza kuchipua mwishoni mwa Januari, hivyo tangu mwezi huo siku za hofu zitaanza na aghalabu zitaendelea mpaka mwisho wa Mei.⁷

Na Mungu Akasema زَلْزَلَةُ السَّاعَةِ , yaani tetemeko hilo litakuwa mfano wa Kiyama. Na tena Akasema:⁸

لَكَ نُورٌ أَيْتٍ وَ نَهْدِمُ مَا يَعْمُرُونَ Yaani Tutaonyesha kwa ajili yako ishara na Tutaendelea kubomoa majengo watakayoendelea kujenga. Kisha akasema: “بھونچال آیا اور شدت سے آیا زمین تہ وہ بالا کر دی” Yaani tetemeko moja

⁶ Ikaja tena rabiū, na likatimia tena Neno la Mungu.

⁷ Sielewi kwamba muradi wa siku za rabiū ni siku zitakazokuja baada ya kupita kipupwe hiki au bishara hii itatimia wakati mwingine ulio wakati wa rabiū. Kwa vyovyote yaonekana kutokana na maneno ya Mungu kwamba zitakuwa siku za rabiū pasipo kujali ni rabiū ipi. Lakini Mungu Atakuja kama mtu anayekuja usiku kwa kujificha, ndivyo Alivyoniambia Mungu.

⁸ Wahyi mmoja wa Mungu kuhusu habari hii ni: Jina langu likang’arika kwa ajili yako.

kali litatokea nalo litazifanya baadhi ya sehemu za ardhi chini juu jinsi ilivyotendeka katika zama za Nabii Luti^{as}. Kasema tena: **يَا أَيُّهَا أَصْحَابُ الْأَنْبِيَاءِ إِنِّي مَعَكُمْ بِعِزَّةٍ** Ya a n i Nitakuja pamoja na majeshi kisirisiri. Hakuna mwenye habari ya siku hiyo jinsi ambavyo kabla ya mji wa Luti^{as}. kupinduliwa hakuna aliyekuwa na habari yake. Wote walikuwa wanashughulikia kula na kunywa na anasa zao mara ardhi ikapinduliwa ghafla. Basi Mungu Anasema ndivyo hivyo itakavyotendeka hapa vilevile, kwani dhambi zimekuwa nyingi kupita mipaka, na wanadamu wameanza kupenda dunia kuzidi kiasi, na njia ya Mungu hudharauliwa. Tena Akasema:

”زندگیوں کا خاتمہ“ .(mwisho wa uhai). Kisha Akasema

Akiniambia:

قَالَ رَبُّكَ إِنَّهُ نَزَّلُ مِنَ السَّمَاءِ مَا يَرْضِيكَ رَحْمَةً مِنَّا وَكَانَ أَمْرًا مَّقْضِيًّا

Yaani Mola wako Asema kwamba jambo moja litashuka kutoka mbinguni nawe utalifurahia. Hii ndiyo rehema kutoka kwetu. Na hilo lilikadiriwa kufanyika tangu mwanzo. Na hakuna budi mbingu ijizuie kushusha jambo hilo mpaka bishara hii ipate kuenea baina ya mataifa. Nani atakayeamini mambo yetu isipokuwa yule aliye na bahati njema. Zingatieni ya kwamba tangazo hilo halina nia ya kueneza tashwishi, bali shabaha yake ni kuzuia hali ya kupatwa na tashwishi baadaye ili asipate kuangamia yeyote pasipo kujua. Kila jambo hufungamana na nia. Basi nia yetu siyo kuudhi, bali ni kuokoa katika udhia. Watubuo watakingwa wasipatwe na adhabu. Lakini mwenye bahati mbaya asiyetubu wala haachani na vikao vya kidhihaka wala hatengani

na maovu na dhambi, siku zake za kuangamia ziko karibu, kwani utundu wake ni kitu cha kukasirikiwa machoni mwa Mungu.

Hapa ingefaa kutaja ya kwamba jinsi nilivyokwishaeleza kabla ya kuwa Mungu Amenipasha habari ya kifo changu. Na Akiniambia Akasema kuhusu maisha yangu ya kwamba “بہت تھوڑے دن رہ گئے ہیں” [Siku chache sana zimebaki].

Na Akasema: “تمام حوادث اور عجائبات قدرت دکھلانے کے بعد تمہارا حادثہ آئیگا” .

[Baada ya kuonyesha matukio yote na maajabu ya kudra ndipo ajali yako itatokea] Hilo laashiria kwamba ni lazima kabisa kabla ya kifo changu dunia ipatwe na mambo kadhaa, na maajabu kadhaa yadhihirike ili dunia itayarishwe kwa ajili ya mapinduzi, na baada ya mapinduzi hayo kifo changu kitokee. Nami nikaonyeshwa mahali fulani kwamba ndipo mahali pa kaburi langu. Nikamwona malaika mmoja akipima ardhi, na alipofika mahali fulani akasema: Hapa ndipo mahali pa kaburi lako! Kisha nikaonyeshwa kaburi moja mahali pamoja ambalo liling’aa zaidi kuliko fedha na udongo wake wote ulikuwa wa fedha. Ndipo nikaambiwa; ‘Hili ni kaburi lako.’ Na nikaonyeshwa mahali pamoja napo pakaitwa ‘Bahishti Maqbara’ (Mava ya Kipeponi) na nikajulishwa kwamba hayo ndiyo makaburi ya watu wema wa Jumuiya watakaokwenda Peponi. Tangu hapo niliendelea kufikiri kununua kiwanja kimoja kwa ajili ya mava. Lakini kwa kuwa viwanja vifaavyo vilikuwa ghali sana, hivyo ununuzi uliahirika kwa muda mrefu. Sasa baada ya ndugu Maulawi Abdul Karim kufariki, nilipofunuliwa mfululizo kuhusu kufariki kwangu pia, nikaonelea kwamba yafaa kufanya mpango wa kupata

kiwanja cha makaburi. Basi nimekitoa kiwanja changu binafsi kilicho karibu na bustani yetu kisichopungua bei yake kuliko Rupia elfu moja. Nami namwomba Mungu Akitilie baraka na kukifanya kuwa Bahishti Maqbara (Mava ya watu wa Peponi), na kwamba kiwanja hicho kiwe ni mava ya wanajumuiya waliotakasika moyo ambao wametanguliza kikwelikweli dini juu ya dunia na wakatengana na mapenzi ya dunia, wakawa kwa ajili ya Mungu na wakajipatia mabadiliko mema ndani mwao na wakaonyesha mfano wa uaminifu na usadiki kama masahaba wa Mtume wa Mungu Sallallahu alaihi wa Sallam. Amin, E Mola wa walimwengu.

Naomba tena ya kwamba E Mungu wangu Muweza, ifanye ardhi hiyo kuwa mava ya waliotakasika nyoyo zao miongoni mwa Jumuiya yangu ambao kwa hakika wamekwisha kuwa wako wala hamna mchanganyiko wa shabaha za kidunia katika mambo yao. Amin, E Mola wa walimwengu.

Naomba tena mara ya tatu kwamba E Muweza wangu Mkarimu, E Mungu Msamehevu Mrehevu, Uwajalie wale tu wapate kuzikwa hapa walio na imani ya kweli juu ya huyu Uliyemtuma wasio na unafiki wala shabaha ya kinafsi wala dhana⁹ mbaya ndani yao, nao wanatimiza wajibu wa imani na utii ipasavyo, na wamekwisha jitolea njiani mwako uhai wao, ambao Umewaridhia, nao ndio wao unaowajua ya kuwa wamejipoteza katika mapenzi

⁹ Dhana mbaya ni balaa kubwa, inayounguza haraka sana imani jinsi moto mkali unavyounguza takataka. Yule anayewadhania vibaya mitume wa Mungu, Mungu Huwa adui wake, na Husimama kupigana naye. Yeye Ana ghera kwa wateule wake sana hata kwamba mfano wake haupatikani. Niliposhambuliwa kwa njia mbalimbali, ghera hiyo ya Mungu ilichemka kwa ajili yangu kama Alivyosema:

yako, na wanaungana na Uliyemtuma kiupendo na kwa kujitolea, kwa uaminifu na adabu kamili na imani ya kibusara. Amin, E Mola wa walimwengu.

إِنِّي مَعَ الرَّسُولِ أَقُومُ وَالْوَمُ مِنْ يَلُومُ دُونَكَ مَا يَدُومُ ذَلِكَ دَرَجَةً فِي السَّمَاءِ وَ فِي الَّذِينَ هُمْ يُبْصِرُونَ. وَ لَكَ نُزِيَّ إِلَيْكَ وَ نَهْدُمُ مَا يَعْمُرُونَ. وَ قَالُوا أَتَجْعَلُ فِيهَا مَنْ يُفْسِدُ فِيهَا. قَالَ إِنِّي أَعْلَمُ مَا لَا تَعْلَمُونَ. إِنِّي مَهِينٌ مَنْ أَرَادَ إِهَانَتَكَ. لَا تَخَفْ إِنِّي لَا يَخَافُ لَدَيْ الْمُرْسَلُونَ. أَنَّى أَمَرَ اللَّهُ فَلَا تَسْتَعْجِلُوهُ. بِشَارَةَ تَلَقَّاهَا النَّبِيُّونَ. يَا أَحْمَدِيُّ أَنْتَ مُرَادِي وَمَعِي. أَنْتَ مِنِّي بِمَنْزِلَةِ تَوْحِيدِي وَ تَفْرِيدِي. وَأَنْتَ مِنِّي بِمَنْزِلَةِ لَا يَعْلَمُهَا الْخَلْقُ. وَ أَنْتَ وَجِيهَةٌ فِي حَضْرَتِي. إِخْتَرْتُكَ لِنَفْسِي. إِذَا غَضِبْتَ غَضِبْتُ وَ كَلَّمَا أَحْبَبْتَ أَحْبَبْتُ. أَتَرَكَ اللَّهُ عَلَى كُلِّ شَيْءٍ. أَلْحَمْدُ لِلَّهِ الَّذِي جَعَلَكَ الْمَسِيحَ ابْنَ مَرْيَمَ. لَا يُسْئَلُ عَمَّا يَفْعَلُ وَ هُمْ يُسْئَلُونَ. وَ كَانَ وَعْدًا مَفْعُولًا لَا يَعْصِمُكَ اللَّهُ مِنَ الْعَذَابِ وَ يَسْطُورُ بِكُلِّ مَنْ سَطَا. ذَلِكَ بِمَا عَصَوْا وَ كَانُوا يَعْتَدُونَ. أَلَيْسَ اللَّهُ بِكَافٍ عَبْدَهُ. يَجِبَالٌ أَوْبِي مَعَهُ وَ الطَّيْرُ كَتَبَ اللَّهُ لِأَعْلِينَ أَنَا وَ رُسُلِي. وَ هُمْ مِنْ بَعْدِ عَابِلِهِمْ سَاعِيُونَ. إِنَّ اللَّهَ مَعَ الَّذِينَ اتَّقَوْا وَ الَّذِينَ هُمْ مُحْسِنُونَ. إِنَّ الَّذِينَ آمَنُوا أَنَّهُمْ قَدِمَ صَدَقٍ عِنْدَ رَبِّهِمْ. سَلَامٌ قَوْلًا مِنْ رَبِّ رَحِيمٍ. وَ امْتَازُوا الْيَوْمَ أَيُّهَا الْمُجْرِمُونَ.

[Tafsiri: Nasimama pamoja na Mjumbe, nami namlaumu akulaumuye. Na nitakupa yatakayodumu mitele. Una daraja kubwa kule mbinguni na baina ya wale walio na busara. Na Tutayonyesha ishara kwa ajili yako na Tutayabomoa wanayoyajenga. Na wakasema: Je Utaweka humu yule atakayeleta ufisadi humu? Akasema: Hakika Najua msiyoyajua. Nitamdhalilisha yule atakayenuia kukudhalilisha. Usiogope, kwani mbele yangu wajumbe hawana hofu. Amri ya Mungu iko tayari kuja, basi msiiharakie. Ni bishara waliyoipata Manabii. E Ahmad wangu, u muradi wangu, nawe u pamoja nami. U kwangu kama ulivyo Umoja Wangu na Upekee Wangu. Nawe una cheo mbele yangu ambacho viumbe hawakitambui. U mhashamu mbele yangu. Nimekuteua kwa ajili yangu. Ughahibikapo naghadhibika. Na kila upendapo nami napenda. Mungu Amekutanguliza juu ya kila kitu. Sifa zote njema zamhusu Mungu Aliyekufanya Masihi bin Maryamu. Yeye Haulizwi kuhusa anachotenda, bali hao huulizwa. Na ndiyo ahadi isiyo na budi kutimizwa. Mungu Atakulinda na maadui, na Atamshambulia kila atakayekusham-bulia. Hayo ni kwa sababu wameasi na kupita mipaka. Je, Mungu Hamtoshei mtumishi wake? Enyi majabali, nyenyekeeni na ndege pia. Mungu Amekwisha kata hukumu kwamba 'Nitashinda mimi na mitume wangu'. Nao baada ya kushindwa watapata ushindi. Hakika Mungu yu pamoja na watawa na wale wafanyao hisani. Hakika wale walioamini watakuwa na daraja kamili mbele ya Mola wao. Salaam – ndilo neno litokalo kwa Mola Mwenye rehema. Na jitengeni leo ninyi wakosefu.

Na kwa kuwa nimepata bishara nyingi sana kwa mava haya, na si tu kwamba Mungu Aliyaita mava ya Kipeponi, bali pia Akasema kwamba **أُنزِلَ فِيهَا كُلُّ رَحْمَةٍ** Yaani kila namna ya rehema imeteremshwa humo, wala hamna rehema ya aina yoyote wasiyoipata sehemu yake wenye kuzikwa humo, hivyo Mungu kwa wahyi wake usio na maneno maalum Akaelekeza moyo wangu kwamba mava hayo yawekewe masharti fulani ili kwamba wale tu wapate kuzikwa humo watakaofuata masharti hayo kwa sababu ya usadiki wao na ukweli wao mkamilifu. Nayo ndiyo masharti matatu; wote watawajibikiwa kuyatimiza:

- (1) Kiwanja cha makaburi kilichopo nimekitoa mimi kama mchango, lakini kwa kukamilisha eneo hili ardhi kiasi fulani itanunuliwa ambayo thamani yake itakuwa Rupia elfu moja takriban. Na ili kukipamba miti itapandwa na kitachimbwa kisima kimoja. Na upande wa kaskazini wa makaburini maji mengi yametulia penye njia, kwa hiyo daraja litatengenezwa hapo. Basi kwa matumizi hayo Rupia 2,000/- zitahitajika. Hizo kwa jumla zimekuwa Rupia 3,000/- zitakazotumika kwa kutimiza kazi hii yote. Basi sharti la kwanza ndilo hili ya kwamba mtu yeyote anayetaka azikwe humo achange cho chote sawa na uwezo wake kwa matumizi hayo. Mchango huu watatoa watu hao tu sio wengine. Kwa sasa mchango huu aletewe ndugu mhashamu Nuruddin. Lakini Mungu Akipenda mchango huu utaendelea hata baada ya sisi sote kufariki, hapo Anjuman (Idara) maalum

yatakiwa ambayo itatumia fedha za mapato haya zitakazoendelea kukusanyika, kwa kueneza ujumbe wa Islam na kuzagaza imani ya Umoja wa Mungu jinsi itakavyoonelea.

- (2) Sharti la pili ni kwamba miongoni mwa wanajumuiya yule tu atazikwa makaburini humu atakayefanya wasia ya kwamba baada ya kifo chake schemu ya kumi ya mali atakayoacha itatumiwa kwa kueneza Islam na kuhubiri maamrishi ya Kurani sawa na maagizo ya Jumuiya hii. Na kila mkweli mwenye imani kamilifu atakuwa na hiari ya kuandika katika wasia wake zaidi yake vile vile, lakini siyo kidogo kuliko sehemu hiyo ya kumi. Mapato hayo yatasimamiwa na Anjuman ya watu waaminifu na wataalam ambao kwa kushauriana pamoja watumia hayo kwa kuendeleza mbele miradi ya Islam na kueneza elimu ya Kurani na vitabu vya dini na pia kwa wahubiri wa Jumuiya hii sawa na maagizo hayo hapo juu. Na Mungu Ameahidi ya kwamba Ataikuza Jumuiya hii, kwa hiyo yatarajiwa kwamba mali nyingi zitakusanyika, na mambo yote yaingiayo katika masilahi ya uenezaji wa Islam ambayo kuyafafanua hayo hivi sasa kutakuwa kabla ya wakati wake, yatatekelezwa kwa mali hizo. Na kundi la watu walio wasimamizi wa kazi hii wakifariki, hapo wale watakaoshika hatamu mahali pao watawajibikiwa kutoa huduma sawa na maagizo ya Jumuiya Ahmadiyya. Katika mali hizo, mayatima, maskini na Waislamu wapya wenye hali ndogo walio Waahmadiyya

pia watakuwa na haki. Na itajuzu kuikuza mali hiyo kwa njia ya biashara. Msidhani ya kwamba hayo ndiyo mambo yasiyowezezana, bali ndiyo matakwa ya yule Mweza Aliye Mfalme wa ardhi na mbingu. Sina wasiwasi ya kwamba mali hizo zitakusanyikaje na kwamba Jumuiya hiyo itapatikanaje ambayo kwa jazba ya uaminifu itajitolea muhanga kufanya kazi hii kubwa, bali nina kiherehere ya kwamba baada ya zama zetu wale watu watakaoachiwa usimamizi wa mali hizo wasije wakateleza kwa kuona wingi wa mali na wakaipenda dunia. Hivyo, naomba ya kwamba daima Jumuiya hii iendelee kuwa na wale waaminifu watakaotumikia kwa ajili ya Mungu. Naam, itajuzu wapewe posho kama msaada wale wasio na mapato yoyote.

- (3) Sharti la tatu ni kwamba mwenye kuzikwa makuburini humo awe mtawa na ajiepushe na yaliyoharimishwa wala asifanye ushirikina wala mambo yoyote yaliyo bidaa. Awe Mwislamu mkweli na safi.
- (4) Kila mtu mwema asiye na milki yoyote, asiyeweza kutoa mali, ikiwa itathibitika kwamba alijitoa wakfu maisha yake kwa kutumikia dini naye alikuwa mwema, aweza kuzikwa makuburini humo.

MAAGIZO

- 1. Kila mmoja anayetaka kufanya wasia sawa na masharti yaliyotajwa hapo juu, wasia wake utatekelezwa baada ya kifo chake. Lakini itamlazimu kuandika wasia na kumkabidhi msimamizi aliyewekwa kwa kuhudumia na pia wasia huu uenezwe kwa kupigwa chapa, kwa sababu mara nyingi kuandika wasia wakati wa kukurubia kifo huwa vigumu. Na kwa kuwa siku za ishara za kimbinguni na mabalaa ni karibu, kwa hiyo mwenye kuandika wasia katika wakati kama huu ana daraja kubwa ambaye anaandika wasia katika hali ya amani. Na yule mfanya wasia ambaye mali yake itadumu kusaidia, thawabu yake nayo itadumu na itakuwa kama sadaka inayo- endelea dawamu.**
- 2. Kila mmoja aishiye mahali pengine mbali na Qadian katika sehemu fulani ya nchi hii naye anafuata masharti hayo hapo juu, warithi wake wanapaswa kuleta maiti yake, baada ya kifo chake, ndani ya sanduku. Na kama mmojawapo akifariki kabla mava hayajakamilika, yaani kabla ya kutengeneza daraja na kadhalika, basi mwenye kuzikwa makaburini humo sawa na masharti apaswa azikwe ndani ya sanduku pale alipofia na kisha baada ya mambo yote kuhusu makaburini kuwa tayari maiti iletwe Qadian. Lakini yule aliyewahi kuzikwa bila kutiwa ndani ya sanduku haitapasa kumfukua kaburini¹⁰**

¹⁰ Mtu asiyeelimika asidhanie mpango huu wa makaburini kuwa bidaa, kwani mpango huu ndio sawa na wahyi wa Mungu, wala siyo kazi ya mtu. Na asidhani yeyote ya kuwa mtu anawezaje kuingia Peponi kwa sababu tu amezikwa makaburini humo. Kwani siyo maana yake kwamba ardhi hii itamfanya mtu kuingia Peponi, bali maneno ya Mungu yanamaanisha kwamba mwenye kwenda Peponi ndiye atakayezikwa humo.

Ibainike ya kuwa Mwenyezi Mungu Amekusudia kwamba waliokamilika kiimani wapate kuzikwa mahali pamoja ili vizazi vijavyo viburudishe imani yao kwa kuona mahali pamoja na ili kazi zao kubwa yaani juhudi walizotia katika shughuli zao za kidini zidumu kujulikana kwa watu.

Hatimaye, twaomba ya kwamba Mwenyezi Mungu Amsaidie kila mwenye ikhlasi katika kazi hii na kumtilia jazba ya kiimani na kuufanya mwisho wao uwe mwema. Amin.

Yamfaa kila mmoja miongoni mwa Jumuiya yetu atakayepata maandiko haya kwamba ayaeneze baina ya marafiki zake na kuyatapakaza kadiri awezavyo na kuyahifadhi kwa ajili ya vizazi vyake vijavyo. Hata wapinzani nao wapashwe habari hizi kwa njia nzuri. Na onyesheni subira mtukanwapo na kila mwenye midomo michafu na endeleeni kuomba dua.

Na mwito wetu wa mwisho ni kwamba sifa zote njema zamhusu Mungu, Mola wa walimwengu.

Mwandishi Mnyenyekevu:

**Mhitaji wa Mungu Ambaye wote wanahitaji kwake:
Ghulam Ahmad – Mungu Amwepushe na kila balaa
na kumsaidia.**

20 Desemba 1905

آلا اے کہ ہشیامدی دپاک زاد ۛ پئے حرص دنیا مدہ دیں بیاد
 بدیں داید فانی دل خود میسند ۛ کہ داد نہاں راحتش صد گزند
 اگر باز باشد ترا گوشش ہوش ۛ زگورت ندائے در آید بگوش
 کہ اے طعمہ من از چند روز ۛ پئے فکر دنیاے دُول کم بسوز
 ہر آن کو بد نیائے دُول مبتلا است ۛ گرفتار رنج و عذاب و غنا است
 برست آنکہ بر موت دارد نگاہ ۛ بریدہ زد دنیا دویدہ براہ
 سفر کردہ پیش از سفر شوے یار ۛ کشیدہ زد دنیا ہمہ رخت و یار
 پئے داید عقبی کمر بستہ چُست ۛ رہا کردہ سامان این خانہ سُست
 چو کایے حیات است کارے نہاں ۛ ہماں بہ کہ دل بگسی زیں مکاں
 جہنم کزو داد فرقاں غیر ۛ ایمل حرص دنیا است جان پدر
 چو آخر زد دنیا سفر کردن است ۛ چو رفتے زیں رہ گذر کردن است
 چرا عاقلے دل بہ بند و دراں ۛ کہ ناگاہ دزد بر گل او خزاں
 بدیں تجمیبستن دل خود خطا است ۛ کہ این شون دین و صدق و صفا است
 چہ حاصل ازین دستانِ دو رنگ ۛ کہ گاہے بصلحت کشند گہ بجنگ
 چرا دل نہ بندی بدایں دستان ۛ کہ ہر ش رہاند ز بند گداں
 برد فکر انجام کن اے غوی ۛ ز معدی شنو گزمن نشنوی

عردسی بود نوبت ماتمت

اگر بر نکونی بود خاتمت

TAFSIRI YA BETI ZA KIAJEMI ZA MWANDISHI

- (1) Ewe ubiabiaye na mwenye tabia njema, usiiharibu dini kwa tamaa za dunia.
- (2) Usitie moyo katika dunia hii itakayotoweka, kwani katika starehe zake mmefichikana mateso mia.
- (3) Kama masikio yako ya kiakili yako wazi, utasikia sauti itokayo kaburini mwako:
- (4) Ya kwamba: Ewe uliye tonge langu baada siku chache, usijiunguze katika hamu ya dunia hii dhalili.
- (5) Kila aliyeifuata-fuata dunia dhalili, atashikwa na huzuni, adhabu na mateso.
- (6) Yule ayaangaliaye mauti yu huru: macho yake mawili yakitengana na dunia huyangoja.
- (7) Kabla hajafa kasafiri kwenda kwa Mpenzi wake, na akatoa mizigo yake kutoka katika dunia.
- (8) Kwa ajili ya Akhera akajiweka tayari kabisa, na akaviachilia mbali vifaa vya nyumba hii mbovu.
- (9) Kwa kuwa maisha haya hayawezi kutegemewa, hivyo yafaa kutenganisha moyo na mahali hapa.

- (10) **Ile Jahanamu ambayo Kurani imetoa habari zake ndiyo tamaa hii ya kidunia, ewe mpenzi.**
- (11) **Kama hatimaye ni kuiaga tu hii dunia na kuipita tu hii njia –**
- (12) **Kwa nini, basi, mwenye akili aipende hiyo, kwani ghafla maua yake yatasibiwa na msimu wa kuyanyausha.**
- (13) **Usiangukie mapenzi ya mkahaba huyo (dunia) kwani huyo ndiye adui wa dini na ukweli na uaminifu.**
- (14) **Utajifaidiaje na huyo mwenye nyuso mbili? Kwani mara hua kwa suluhisho na mara kwa vita.**
- (15) **Mbona hufungamani kimoyo na Mpenzi yule ambaye mahaba yake hukuachisha huru!**
- (16) **Nenda ukafikirie mwisho wako, mpotevu we! Kama hunisikilizi, tega basi masikio kwa aliyosema Sa'di:**
- (17) **Wakati wa kukuomboleza utakuwa kama wakati wa arusi yako kama mwisho ukiwa mwema.**

NYONGEZA YA KIJITABU 'WASIA'

Kuhusu kijitabu cha WASIA kuna baadhi ya mambo yanayofaa kuenezwa ambayo yanaandikwa hapa chini:

- (1) Kwanza ni kwamba kabla Anjuman Karpardaz (Kamati ya utendaji) kuhusu masilahi ya makaburini haijatangaza kwamba kiwanja cha makaburi kipo tayari kikamilifu kwa kila jiha, haitajuzu kuleta hapa maiti ya yule aliyetimiza masharti ya kijitabu cha 'Wasia' kwa kuzikwa makuburini humo. Bali hapana budi kwanza daraja na mapasiko mengine yawe tayari. Mpaka wakati huo maiti itazikwa kwa muda katika mava mengine yoyote kwa kutiwa ndani ya sanduku.**
- (2) Mtu yeyote mwenye kukiri kutimiza masharti ya kijitabu cha 'Wasia' atalazimika ya kwamba mashahidi wawili kwa akali washuhudie kukiri kwake na ailetee Anjuman wasia wake akiwa mwenye akili timamu. Na afafanue kwa uwazi ya kwamba yeye anatoa kama wasia au wakfu sehemu ya kumi ya milki yake yote, inayoweza kuhamishika au isiyoweza kuhamishika, kwa kueneza miradi ya Jumuiya ya Ahmadiyya. Na italazimu kutangaza wasia huo kwa uchache katika magazeti mawili.**
- (3) Anjuman itawajibikiwa kumtolea mwenye kufanya wasia hati iliyotiliwa saini na muhuri wa Anjuman baada ya kuchunguza vizuri maneno ya wasia ki-kanuni na kisheria. Na maiti yoyote ikiletwa makaburini sawa na kanuni hizo hapo**

juu, hati hiyo ionyeshwe na kisha maiti izikwe sawa na maagizo ya Anjuman mahali pale palipowekwa na Anjuman kwa mazishi yake.

- (4) Katika kiwanja hiki cha makaburi watoto wasiopata kubalehe – isipokuwa kwa subabu maalum itolewayo na Anjuman – hawatazikwa, kwani hao ndio waendao Peponi mapema; wala jamaa yeyote mwingine wa maiti hataweza kuzikwa humo mpaka jamaa huyo mwenyewe apate kutimiza masharti yote ya kijitabu cha ‘Wasia’.
- (5) Yeyote asiyefia humu Qadian, maiti yake haitajuzu kuletwa hapa Qadian pasipo kuwekwa ndani ya sanduku. Aidha hakuna budi habari yake iletwe kwa uchache mwezi mmoja mapema ili kama vikwazo fulani vikizuka ghafula kuhusu mava, Anjuman iweze kuviondolea mbali kabla ya kutoa ruhusa.
- (6) Kama mmojawapo akifariki, Mungu Apishe mbali, kwa maradhi ya tauni, ambaye amekwisha timiza masharti ya kijitabu cha ‘Wasia’, basi kumhusu yeye inaagizwa ya kwamba huyo azikwe mahali pengine ndani ya sanduku kwa miaka miwili kama amana. Kisha baada ya miaka miwili maiti hiyo iletwe Qadian wakati ambapo katika mahali pa kufia kwake na huku Qadian tauni hakuna.
- (7) Izingatiwe ya kuwa haitatosha kutoa tu sehemu ya kumi ya milki inayoweza kusogezwa na isiyoweza kusogezwa, bali itamlazimu mwenye kufanya wasia, kadri awezavyo, awe anatekeleza maamrishi yote ya Islam na kujibidiisha katika

mambo ya ucha-Mungu na utakaso; na awe Mwislamu, mwenye kumwamini Mungu kwamba Yu Mmoja, na amwamini Mtume Wake barabara wala asiwe mwenye kunyanganya haki za watu.

- (8) Kama mtu amefanya wasia kutoa sehemu ya kumi ya milki yake, kisha kafa kwa kughariki mtoni au kafia nchi nyingine ambako kutoka huko kuleta maiti ni shida, hapo wasia wake utakuwa utasihi na mbele ya Mungu atahesabiwa kana kwamba amezikwa makaburini humu; na itajuzu kuandika habari zake juu ya tofali au jiwe na kulijengea makaburini humu.
- (9) Anjuman itakayosimamia fedha hizo haitakuwa na hiari ya kuzitumia popote isipokuwa kwa miradi ya Jumuiya Ahmadiyya. Na katika miradi hiyo yote uenezaji wa Islamu utatambulizwa. Na itajuzu kuzikuza fedha hizo kwa njia ya biashara baada ya Wana-Anjuman kushauriana pamoja.
- (10) Wana-Anjuman wote watakuwa wale walio Waahmadiyya nao ndio weye tabia njema na waaminifu. Na kama baadaye ikionekana kumhusu mmojawapo kwamba hana tabia njema au si mwaminifu au kwamba yu mdanganyifu na mpenzi wa mambo ya kidunia, basi Anjuman itawajibikiwa kumwondoa haraka na kumweka mwingine mahali pake.
- (11) Kama matata yakizuka kuhusu mali ya wasia, basi matumizi yote ya kesi hiyo yatalipwa kutoka katika mali hiyo ya wasia.
- (12) Kama mtu baada ya kwisha kufanya wasia

akikataa wasia wake kwa sababu ya udhaifu fulani wa imani yake au akiiacha Jumuiya hii, hapo licha ya kuwa Anjuman imekwisha chukua mali yake kisheria, haitajuzu kuwa na mali hiyo; bali mali hiyo yote arudishiwe kwani Mungu Hahitaji mali ya mtu yeyote; bali mali kama hiyo huchukiza na yafaa kukataliwa.

- (13) Kwa kuwa Anjuman ni naibu ya Khalifa aliyewekwa na Mungu, hivyo Anjuman hii haina budi kutengana kabisa na mawaa ya kidunia na mambo yake yanapaswa kuwa safi sana na juu ya msingi wa uadilifu.
- (14) Itajuzu ya kwamba ili kuipa nguvu Anjuman hii na kuisaidia, Anjuman nyingine ziwepo katika nchi za mbali zilizo chini ya Anjuman hii. Na itajuzu ya kuwa kama hizo ziko katika nchi ambako kutoka huko kuleta maiti ni shida, basi, maiti izikwe huko huko, na ili kupata thawabu, mtu huyo kabla ya kufa afanye wasia wa kutoa sehemu ya kumi ya mali yake. Na kuchukua mali za wasia ndiyo wajibu wa Anjuman ile iliyopo katika nchi hiyo. Na itafaa kutumia fedha hizo katika nchi hiyo hiyo kwa miradi ya kidini. Na itajuzu, ikitokea haja, kuipatia fedha hizo Anjuman hii ambayo makao yake makuu ndiyo Qadian.
- (15) Ni wajibu ya kwamba makao ya Anjuman hii yawe Qadian daima dawamu, kwani Mungu Ameibariki. Itajuzu pia ya kwamba sawa na mahitaji ya siku zijazo jengo la kutosha lijengwe kwa shughuli hizi.
- (16) Katika Anjuman kwa uchache Wana-Anjuman

wawili lazima wawepo ambao wana ujuzi wa Kurani na Hadithi barabara nao ndio wajuzi wa lugha ya Kiarabu na elimu ya vitabu vya Jumuiya Ahmadiyya.

- (17) Kama, Mungu Apishe mbali, yule anayefanya wasia sawa na kijitabu cha 'Wasia' ni mwenye ukoma ambaye hali yake ya kimwili haistahili aletwe makaburini humu, basi sawa na masilahi ya kidhahiri haitafaa huyo aletwe katika mava haya; lakini akiimarika juu ya wasia wake atajaliwa daraja lile lile alipatalo mwenye kuzikwa humu.
- (18) Kama mtu hana milki inayoweza kuhamishika wala isiyoweza kuhamishika, lakini imethibitika juu ya hayo kwamba yu derweshi mwema na mtawa na mwaminio halisi wala hana sehemu ya unafiki au mapenzi ya dunia au kasoro ya utii ndani yake, basi huyo naye kwa idhini yangu au baada yangu kwa shauri ya pamoja ya Anjuman anaweza kuzikwa humu.
- (19) Kama mtu fulani akikataliwa na wahyi maalum wa Mwenyezi Mungu, yeye mtu huyo hataingia makaburini humu, hata kama akifanya wasia wa kutoa mali yake.
- (20) Mimi, mke wangu na watoto wangu tumetengwa na Mungu. Mwingine yeyote awaye, akiwa mwanamume au mwanamke, analazimika kutimiza masharti hayo; na mwenye kubisha atakuwa mnaiki.

Hayo ndiyo masharti ya lazima yaliyoandikwa hapo juu. Tangu sasa yule tu atazikwa makaburini humu

atakayetimiza mashrti hayo. Yawezekana kwamba baadhi ya watu waliotawaliwa na dhana mbaya watupinge kwa sababu ya jambo hili na waufikirie mpango huu kwamba msingi wake ni shabaha za kibinafsi au wauhesabu kuwa bidaa lakini ikumbukwe ya kuwa hizi ni kazi za Mwenyezi Mungu; Hufanya Apendavyo. Bila shaka Amekusudia kuwapambanua wanafiki na waaminio kwa njia ya mpango huu. Nasi twahisi ya kwamba wale ambao wakipata habari za mpango huu wa Mungu hushughulikia bila kukawia kutoa sehemu ya kumi ya milki yao katika njia ya Mungu, bali huonyesha jazba nyingi zaidi kuliko kiasi hicho, hao wanapiga muhuri juu ya uaminifu wao. Mwenyezi Mungu Asema:

الْمَ أَحْسِبَ النَّاسُ أَنْ يُتْرَكُوا أَنْ يَقُولُوا آمَنَّا وَهُمْ لَا يُفْتَنُونَ

“Je watu wanadhani ya kwamba Nitaridhika kwa kadri hii tu ya kuwa waseme kwamba tumeamini nao wasitahiniwe bado.” Na mtihani huu si chochote. Masahaba walitahiniwa kutoa uhai wao, nao wakajitolea na wakapata kuuawa katika njia ya Mungu. Basi fikira hii ya kuwa kwa nini watu wote kwa jumla bila masharti wasiruhusiwe kuzikwa makaburini humu, ni mbali nmamna gani na uhakika wenyewe! Kama hiyo ndiyo sawa, kwa nini, basi, Mwenyezi Mungu Aliweka msingi wa mtihani katika kila zama? Alitaka katika kila zama kwamba Awapambanue wabaya na wema. Kwa hiyo, sasa pia Amefanya vivyo hivyo. Katika zama za Mtume^{sa} Mwenyezi Mungu Aliweka pia mitihani midogo midogo. Kwa mfano ilikuwa desturi ya kuwa mtu yeyote asishauriane na Mtume ^{s.a.w.} kabla hajatoa

zawadi. Basi hiyo nayo ikawa jaribio kwa wanafiki. Tunatambua ya kwamba kwa njia ya mtihani wa wakati huu pia watapambanuka wenye ikhlasi ya hali ya juu waliotanguliza kikweli dini juu ya dunia mbali na watu wengine. Na itathibitika ya kwamba wametimiza ahadi ya baiati na kudhihirisha ukweli wao. Hakuna shaka ya kuwa mpango huu utakuwa mzito kwa wanafiki nao wataaibika; na baada ya kufa – wakiwa wanaume au wanawake – hawatapata kuzikwa makaburini humu.

فِي قُلُوبِهِمْ مَّرَضٌ فَزَادَهُمُ اللَّهُ مَرَضًا [Mioyoni mwao mna maradhi, na Mungu Amewazidishia maradhi. 2:11] Lakini watanguliao katika habari hii watahesabiwa wakweli nao watadumu kupata rehema milele.

Hatimaye, ikumbukwe pia ya kwamba siku za mabalaa zi karibu, na liko karibu tetemeko moja kali sana litakalofanya ardhi chini juu. Basi wale watakaohakikisha kuwa wametengana na dunia na kuthibitisha kwamba wametekeleza namna gani agizo langu, hao ndio waaminio wa kweli mbele ya Mungu, nao ndio watakaoandikwa katika daftari yake kuwa watangulizi wa kwanza. Nasema kwelikweli ya kwamba zama zi karibu ambapo mnafiki ambaye kwa kuipenda dunia akapuuza agizo hilo, atasema kwa masikitiko wakati wa kuadhibiwa kwamba laiti ningalitoa milki yangu yote – iwezayo kuhamishika na isiyoweza kuhamishika – katika njia ya Mungu na kusalimika katika adhabu hii. Angalieni; nawapasheni habari ya adhabu iliyo karibu sana. Jikusanyieni masurufu haraka sana ili yawafae. Sitaki nichukue mali yoyote kutoka kwenu na kuifanya milki yangu; bali mtaitolea Anjuman moja

ya kumi ya mali yenu kwa kueneza dini na mtapata maisha ya Peponi. Ni wengi watakaoepa amri yangu kwa kuipenda dunia, lakini haraka sana watatengwa mbali na dunia, ndipo wakati wa mwisho watasema:

هَذَا مَا وَعَدَ الرَّحْمَنُ وَصَدَقَ الْمُرْسَلُونَ

[Hayo ndiyo Aliyoahidi Rahmani, na Mitume walisema kweli 36:53].

Salamu iwe kwa wafuatao mwongozo .

Mwandishi mnyenyekevu,
 Mirza Ghulam Ahmad,
 Masihi Mau'udi kutoka kwa Mwenyezi Mungu
 Januari 6, 1906
 (Gazeti la Al-Hakam, J 10, Toleo 2
 la 17 Januari 1906)



**TAARIFA YA KIKAO CHA KWANZA CHA
MAJLIS MU'TAMADIN
SADR ANJUMAN AHMADIYYA
KILICHOFANYIKA 29 JANUARI 1906**

WALIOHUDHURIA KATIKA KIKAO

- Hadhrat Maulawi Nurud dinMwenyekiti;
 - Khan Sahib Muhammad 'Ali Khan,
 - Sahibzada Bashiruddin Mahmud Ahmad,
 - Maulawi Sayyid Muhammad Ahsan,
 - Khwaja Kamaluddin;
 - Dakta Sayyid Muhammad Husain; Katibu wa Kamati;
- Kwa kuwa ilikuwa hakuna budi kutoa baadhi ya maagizo ya muhimu na kutoa kibali kwa mambo kadhaa, na nafasi ya kutosha ilikuwa hakuna kuwaarifu ndugu wakaao sehemu nyingine, hivyo kwa idhini ya Hadhrat Imam^{as}. kikao hiki kiliitishwa baada ya kukubaliwa kanuni.

MAAZIMIO YAFUATAYO YALIPITISHWA

- (1) Iliazimiwa ya kwamba muswada wa Wasia uliopendekezwa..... utolewe kibali.
- (2) Iliazimiwa ya kwamba hivi sasa nakili 800 za muswada wa Wasia zichapishwe nao pia utangazwe katika magazeti ya Al-Hakam na Badr.

-
- (3) Iliazimiwa ya kwamba wafanyao wasia wapelekewe maagizo yafuatayo ili yatekelezwe, na pia yacha- pishwe hayo maagizo chini ya fomu ya wasia:
- a) Kama wakihitaji wafanyao wasia waombe kupelekewa muswada wa wasia..... na waandike upya katika karatasi ya kawaida. Na popote palipoachwa nafasi waijaze ipasavyo. Karatasi imara itumiwe kwa kuandika wasia.
 - b) Kadri iwezekanavyo wasia usajiliwe. Na pia ikiwezekana wasia utiliwe saini za warithi au washiriki wa mfanya wasia kama mashahidi; na pamoja nao saini za waheshimiwa wawili wa mji au kijiji zitiliwe vile vile.
 - c) Mfanya wasia na kadhalika mashahidi hata kama wanajua kusoma na kuandika ama sivyo hawana budi kutia alama ya kidole gumba pamoja na sahihi au mihuri yao. Wajuao kusoma na kuandika watatia saini vilevile Mwanamume atatia alama ya kidole gumba cha mkono wa kushoto na mwanamke kile cha mkono wa kuume.
 - d) Mfanya wasia akijua kuandika apaswa aandike kwa mkono wake mwenyewe.
 - e) Hakuna haja ya kubandika stampu juu ya wasia.
 - f) Mfanya wasia akiwa na sababu maalumu inayohitaji mashauri ya kisheria, basi amwandikie barua.... aliye mshauri wa kisheria wa Anjuman na kupata mwongozo.

- (4) Kama wenye ardhi mkoani Panjab wakiwa na matatizo kwa kufanya wasia, yafaa kwamba ile sehemu ya ardhi wanayotaka kufanya wasia wake waitoe katika uhai wao kwa sura ya hiba. Na juu ya hati ya hiba wachukue saini za wale wanaotazamiwa kuwa warithi wao (kama hao wapo) ili ifahamike kwamba hao warithi wameridhia. Na kusajili hati ya hiba ni jambo la lazima. Milki iliyotolewa kama hiba lazima isajiliwe. Na mwingilio na mrudio wa hiba hiyo uwe kwa jina la Sadr Anjuman Ahmadiyya. Lakini hapo watatakiwa kufanya kila mara hivyo pindi wapatapo milki mpya.
- (5) Kama hiba iliyotajwa katika azimio la 4 pia ina matatizo, hapo ardhi yoyote wanayotaka kutoa kama wasia au hiba iwekewe bei yake au iuzwe na thamani yake itolewe kwa Majlis Karpardaz Masalih Qabristan (Kamati ya utendaji wa masilahi ya Makaburini). Lakini kila mara wakipata ardhi mpya itafanywa vivyo hivyo.
- (6) Wale wasio na milki (ardhi, nyumba n.k.), lakini wana mapato kwa njia fulani, basi waitolee Anjuman sehemu ya kumi kwa uchache kila mwezi. Ni hiari yao kuihesabu michango wanayotoa hivi sasa kwa kuisaidia Jumuiya tukufu katika sehemu ya kumi ama kuiweka mbali. Lakini wakitaka kuihesabu ndani ya sehemu ya kumi, hapo waendeleo kuleta kama kawaida na kisha waitoe katika mchango wa wasia na kiasi kilichobakia wakilete kwa Bwana fedha wa Majlis Karpardaz Masalih Qabristan.

Kwa mambo mengine waandikiane na katibu wa Majlis. Lakini watalazimika kufanya wasia ya kuwa baada ya kifo chao sehemu ya kumi kwa uchache ya urithi wao itamilikiwa na Anjuman.

Ukumbusho (1): Wapendao kujua zaidi kanuni kuhusu wasia au hiba kwa Majlis Karpardaz Masalih Qabristan wamwandikie..... kabla ya kuandika wasia au hati ya hiba.

Ukumbusho (2): Katika hali mahususi mwaweza kuandikiana na Majlis Mu'tamadin kwa kufahamiana na kuafikiana kuhusu jambo fulani.

- (7) Fedha zote za mchango wa makaburini au zilizo sawa na tangazo la wasia ilivyoelezwa hapo juu ziletwe kwa anuani hii tu:
“Bwana Fedha, Majlis Karpardaz Masalih Qabristan.” Wala zisiletwe kwa jina la mtu yeyote ama kwa anuani yoyote.

Mnyenyekevu
Muhammad Ali, Katibu
29 Januari 1906

(Saini ya Hadhrat Masihi Mau'udi^{as})
Mirza Ghulam Ahmad

Nuruddin 1 Julai 1906